

Uhakiki kati ya marekebisho na ubomoaji

Mwanzo kabisa hatuna budi kutenganisha kati ya uhakiki ulio mzuri na ule mbaya, Na kinyume chake ambacho ni ubomoaji. Maana ya neno la kwanza nalo limechukuliwa katika mfano ule wa kusema “ dhahabu na fedha zimesafishwa” ikimaanisha kuwa zimetenganishwa kati ya dhahabu / fedha nzuri na ile siyo nzuri. Na maana ya neno la pili likiwa na maana ya ubomoaji (maporomoko) ni kama kusema “mtu Fulani amefariki chini ya maporomoko: ikiwa na maana yupo chini ya mabaki ya nyumba iliyoyabomoka.

Na neno uhakiki katika lugha lina maana mbili: ya kwanza: aibu, tusi na lawama, mfano kama alivyosema Abi Dardai (Mwenyezi Mungu amwie radhi) “ukiwatusi watu nao watakutusi na ukiwaacha nao watakuacha: ikiwa na maana iwapo utawatia aibu na lawamani nao pia watafanya hivyo, kwani iwapo kama una ulimi basi watu wana ndimi.

Ama maana ya pili ni ile inayokusudiwa ya kupambanua kati ya jema na baya, inaweza kuwa ni kusifia na kupendezeshea na inaweza kuwa pia kukejeli na kutusi na inaweza kukusanyika ikakusanya yote mawili.

Na uhakiki unaweza kuwa ni wa kibinafsi au wa kitabia, na unaweza kuwa ni wa kielimu na kimitaala na kimaudhui. Mfano wa uhakiki wa kibinafsi ni; kwa mfano kusoma makala au kusikiliza hotuba au neno au hadithi au kuona ubao ulochorwa na fanani na ukashangazwa nao bila ya kutaka kujua undani wa fani

au kujua sababu za uzuri wake, na unaweza usishangazwe kwa kutotaka kujua undani wa fani ile ambayo kwa mtazamo wako haina kiwango cha uzuri.

Ama kwa upande wa uhakiki wa kielimu na kimitaala na maudhui ni ule uliopo na uliosimamia misingi ya kielimu na kimaudhui na kifani na uhakiki wa namna hii unahitaji nguzo tatu kuu:–

Nguzo ya kwanza: Zana zenye kuhusika na utengenezaji au fani. Mhakiki wa kazi za ufasihi anahitajika kujua sana lugha kwa mfano nahau, sarufi, elimu ya mashairi, elimu ya ufasaha wa usemajji, na elimu ya uhakiki, na fasihi pamoja na kujua baadhi ya elimu nyengine za kibinaadamu, kijamii, kisaikolojia, fani za historia , ustaarabu wa jamii na ujenzi na masome mengine kwa ujumla. Mhakiki wa mahesabu au wa kisiasa au wa fani au uchoraji hana budi kuwa na kiwango kikubwa sana cha misingi ambayo anataamali nayo. Kinyume chake atakuwa anafanya uhakiki wa kijuujuu tu na atahitajika kuwepo wa kumhakiki na wa kumkosoa pia, na pengine afikwe na kejeli kutoka kwa atakaemueleza vibaya na hata kumdharau.

Nguzo ya pili: kwa mhakiki awe na utambuzi na ujuzi na umiliki, je huoni kuwa unaweza kusikia msomaji anasifia hutuba mbili nzuri zenye mvuto mkubwa au ukasoma vitabu viwili vya makala vya waandishi wakubwa ukawa una zana zote za ufahamu (inakusudiwa elimu kwa fani tafauti) au ukapata kuhakiki kazi za kielimu na kifani zilizo na ufanisi wa hali ya juu, isipokuwa unaweza ukapambanua kazi hizo kwa kitu chenye kufahamika lakini ikawa ni vigumu kuelezeka. Mfano kama alivyosema Al Amindiy: “ huoni kuwa unaweza kukutia farasi wawili wazuri wakawa na sifa zilizofanana kwa upande wa uhodari werevu

na nguvu na uasili na ikawa kwa mwenye akili ni vigumu kuwapambanua, isipokuwa kwa wale wenye ujuzi wa farasi kwao ikawa wanaweza kuwatenganisha mmoja kutoka mwengine, vile vile mbao zilizochorwa kwa ustadi mkubwa na majengo yaliyojengwa kwa kiwango kwa wenye ujuzi ni rahisi kujua uzuri uko wapi na kasoro iko wapi kwa kuwa wanamiliki zana za utambuzi wa fani hiyo.

Ama kuingilia tu fani ya uhakiki kwa wasio na ujuzi nayo na wala wasio miliki zana zake au hata kuisomea hili huwa ni tatizo kubwa ambalo hucheleweshwa na lisiloleta maendeleo na lenye kuharibu na lisilojenga na humpa sifa mbaya mhakiki kabla ya alichokihakiki.

Nguzo ya tatu: nayo ni muhimu sana nayo ni kutenda kwa moyo wote na kujiepusha na matamania na kusifika kwa watu, kwani kuingia katika matatizo na matamania na kuacha kutenda yanayotakikana ni janga kubwa ambalo inapasa kujiepusha nalo. Hii ni kwa kuwa baadhi ya nyoyo ni gonjwa hazielewi isipokuwa njia ya ubomoaji pekee na kama alivyosema Imamu Ali Bin Abdiaziz Al jarjani katika utangulizi wa kitabu chake, kinachoitwa *Alwasatwatu baina almutanabiy wakhusumu*. Ametaja kuwa upungufu upo wa makundi mawili: kundi hufanya kwa ajili ya kurekebisha mapungufu yao na kuficha aibu, na jambo hili ni jema kwa kuwa mhakiki amejishughulisha zaidi na nafsi yake na kujaribu kujiweka katika nafasi nzuri. Ama kundi la pili ni la wale wenye mapungufu ikawa wamejikali ima kutokana na kushindwa au kwa hiyari yao au kwa udhaifu au kwa uvivu na hakuna kitu kinachowalazimisha wawe na mapungufu au kuweza

kuhifadhi aibu zao kutokana na mapungufu hayo, na wakawa wanadhania kuwa na mwenendo huo kutawafanya waweze kunyanyuka na kupata vyeo vya juu. “

Na wengi wamefikwa na jaribio hili hata katika zama zilizotangulia ikawa wanachumia pato lao kwa kupitia sifa wanazosifiwa na maneno mazuri wanayopambiwa, na kujipatia pato kwa njia ya kusifiwa jambo hili lilikuwa ni maarufu tangu zama za kijahili kwani wapo waliojulikana kama chuo cha utunzi au cha uchumaji kupitia mashairi kwa mfano Zuheyri bin Abi Salma, Nabia Adhubiyan na wengineo, na wengine walijulikana kwa ufasaha hata mwanzoni mwa kuja kwa uisilamu kama Hutwaya ambae alikuwa akiwatishia watu kutokana na ufasaha wake wa kuweza kumsema mtu vibaya, mpaka kiongozi Umar (Mwenyezi Mungu amwie radhi) akamtishia sana pindi asipoacha kuhujumu tabia za watu, akasema: “ basi na wafariki watoto lakini nitanunua kutoka kwake (Hutwaya) heshima za watu kwa dirhamu elfu arobaini ili asije akamvunjia heshima yeyote. Na Hutwaya akaacha kuwakejeli watu kwa muda wa uongozi wa Umar kisha akarudia tena baada ya kufariki kwake.

Haya yote hayawezi kutengeneza ustaarabu wa kweli au kuendelea kwa jamii yenye usawa ambayo inastahiki kusifiwa na pongezi za kweli, lakini uhakiki wa aina hii hubomoa. Na uhakiki wa kweli wa kimaudhui uliojengeka kwa misingi ya kielimu na ujuzi wa utaalamu na uadilifu huu ndio utakaojenga. Kwa mfano kusema kwa aliyefanikiwa: “ umefanikiwa” na kwa aliyekosea, kumwambia kwa heshima kuwa “umekosea na umepunguza. kwani huenda akajirekebisha na kuitafuta njia ilizo sawa. Na huu ndio uhakiki wenye malengo ambao haubomoi

bali hujenga na wenye uadilifu na kushajiisha na wakati huohuo unaweka wazi pamoja na kutahadharisha.

Na iwapo uongozi ni majukumu na ni amana basi kuhakikisha uhakiki na uchambuzi ni amana na majukumu vilevile. Nasi sote tutaulizwa mbele ya Mwenyezi Mungu Mtukufu. Kila mtu ataulizwa juu ya amana ambayo Mwenyezi Mungu amempa. Kama ambavyo tutaulizwa juu ya ujenzi wa taifa letu na kazi za uimarishaji wake na ukuaji wake kupitia njia za ujenzi na marekebisho na si kwa njia za uvunjaji na ubomoaji. Na si kwa njia ya kujinufaisha au kupenda kuonekana, kwa wengi wetu sasa wanaweza kutambua nini ngano na nini pumba. Na Mwenyezi Mungu anasema katika kitabu chake kitukufu: **“Basi lile povu linapita kama takataka tu basi. Ama kinacho wafaa watu hubakia kwenye ardhi.**